*Mulika, Na. 42 (1), 52-65*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Mhusika Sauti katika Tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* ya Said A. Mohamed

*Collins Kenga Mumbo*[1]
na
*Anne Mwari*[2]
Chuo Kikuu cha Moi

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na42t1.4

**Ikisiri**

Makala haya yanalenga kudadisi sauti na uhusika wake kwenye uwasilishaji wa ujumbe katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* ya Said A. Mohamed (2011). Sauti kama mojawapo ya vipengele vya utendaji imetumiwa katika kazi tofautitofauti za tamthilia kwa sababu mbalimbali kutegemea mahitaji ya mtunzi wa kazi ya sanaa. Sauti inaweza kutekeleza jukumu kubwa inaposhirikishwa vilivyo katika tamthilia. Hata hivyo, watunzi wengi wanatumia sauti kwa ajili ya kushereheshea jambo fulani, kusisitizia ujumbe na kutoa maoni kuhusu wazo kuu linalolengwa hadhira. Wakati mwingine sauti huwa inatumika kama kicheko au kuweka utangulizi na kuhitimishia tamthilia. Kwa kuzingatia matumizi hayo, ni bayana kuwa matumizi ya sauti katika tamthilia nyingi bado hayajapewa uzito unaostahili. Kutokana na hali hiyo makala haya yanachunguza namna sauti ilivyotumika kama mhusika na uwasilishaji ujumbe kwa kurejelea tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya*. Hivyo, mbinu iliyotumika kukusanya data za utafiti huu ni usomaji wa kina wa tamthiliya tajwa. Hii ni tamthilia ya kipekee katika matumizi ya sauti, ambapo mwandishi Said A. Mohamed amewajenga baadhi ya wahusika wake kama wahusika sauti. Amezifanya sauti sio tu kuongea bali pia kushiriki kikamilifu katika majibizano na uigizaji na wahusika wengine. Tumezingatia jinsi sauti ilivyotumika kujenga na kukuza wahusika na uhusika katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* kwa kujikita katika ushiriki wa mhusika binafsi, uhusika wa makundi na njia zinazotumiwa na wahusika sauti kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa na mwandishi. Hatimaye, tumetathmini mchango wa sauti hizi katika kufanikisha utendaji na uwasilishaji maudhui kwa hadhira lengwa.

## 1.0 Utangulizi

Sauti ni mlio unaotoka katika kinywa cha mwanadamu wenye shabaha ya kuwasilisha ujumbe fulani kwa watu. Sauti ni nyenzo muhimu ya mawasiliano ambayo hutumika katika miktadha mbalimbali kama vile katika uwasilishaji wa tamthilia, masimulizi ya kitathmini, matangazo ya biashara na ukalimani. Sauti

---

[1] Baruapepe: kengamumbo15@gmail.com

[2] Baruapepe: annesteve91@gmail.com

katika utendaji wa tamthilia inatumika ili kutekeleza shabaha maalum na kuleta athari muhimu za kisanii katika tamthilia. Athari hizi mara nyingi hukusudiwa kuibua hisia fulani miongoni mwa hadhira, washiriki ama wasanii. Athari zinazoibuliwa zinaweza kuwa za kimwili, kimazingira, kiutambuzi na kisaikolojia. Mara nyingi sauti zinapotumika katika utendaji wa kidrama hutolewa moja kwa moja na mhusika au kupitia vyombo vya kielektroniki. Ijapokuwa tumesema sauti ni milio, kuna milio mingine ambayo si sauti, kwa mfano milio inayotokana na vitu kugusana au kusuguana kama vile kugongana, kupigana, kukwaruzana, kuchapana, kukereza, kuanguka, kupasuka na kulipuka. Kuna milio ya mvua inaponyesha, kuna mingurumo inayoambatana na radi, kuna mingurumo ya magari na mitambo mingine. Iko milio inayotolewa na viumbe kama vile ndege, wanyama wanaofugwa na wanyama wa porini. Milio hii yote haisadifu kuwa sauti kwa sababu iko nje ya mawasiliano ya mwanadamu.

Goldfarb na Wilson (2002) katika ufafanuzi wa sababu za matumizi ya sauti katika drama, wanabainisha sababu mbili za msingi zinazolazimu matumizi yake katika utendaji. Kwanza, ni kuleta athari za kimazingira na athari nyinginezo zinazohitajika katika utendaji; na pili, sauti hutumika kusisitiza yanayozungumzwa au yanayotendwa katika utendaji wa kimelodrama. Wanaeleza ya kwamba sauti zinazosikika nje ya mahali alipo mtendaji huwa muhimu zikijumuishwa katika utendaji. Hizi ni sauti za kimazingira ambazo ni sehemu ya maisha ya kila siku ya mwanadamu.

Ili kufanikisha ujenzi wa baadhi ya athari za kidrama katika tamthilia, mwandishi anaweza kutumia sauti pamoja na milio kama vile Said A. Mohamed alivyofanya katika *Kimya Kimya Kimya.* Mathalani, ametumia mlio mkali unaotokana na kuanguka kwa vitu vya chuma jikoni ili kubadili mkondo wa matukio. Tukio hilo limefanyika wakati Bw. Binafsi alipokuwa amekasirishwa na binti yake Mpya. Mlio huo mkali ulimfanya kuelekeza hasira zake mahali kwingine japo kwa muda mfupi.

Katika makala haya tumefafanua dhana za tamthilia na drama huku tukionesha tofauti iliyopo kwa sababu wanataaluma na wasanii mara nyingi huwa wanazichanganya na kuzitumia kwa pamoja. Kwa mfano, Habwe na Zaja (2019) wanaelezea tamthilia kama dhana ya kifasihi inayotumiwa kurejelea utanzu na kazi za kidrama au michezo ya kuigiza kwa jumla. Japo tamthilia inawasilishwa kwa njia ya maandishi, kimsingi huwa inatungwa kwa kuigizwa hadharani mbele ya hadhira. Wamitila (2003) anaielezea tamthilia kama kazi ya kidrama na ya kimaongezi ambayo huigizwa mbele ya hadhira au kazi inayoandikwa ili kusomwa. Ukizingatia vijelezi hivi viwili kwa makini utabaini ya kwamba istilahi za tamthilia na drama zinatumika sambamba kana kwamba ni kitu kimoja ilhali ni tofauti. Wote hawa katika ufafanuzi wao wanakubaliana ya kwamba tamthilia ni kazi ya kidrama, sasa swali linalojitokeza ni, je drama ni nini? Labda tunaweza kurudi palepale pa kuambiwa ni maigizo ya kitamthilia! Uchunguzi huu unaiangazia tamthilia kama

mtungo wa kisanaa wenye kutumia lugha ya majibizano ili kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira. Katika tamthilia, matukio huzungumziwa kwa kutumia kauli za majibizano baina ya wahusika au washiriki. Lengo kuu la tamthilia huwa ni kuigizwa mbele ya watu, yaani kuwasilishwa jukwaani au mahali popote pa wazi ambapo watazamaji wanaweza kushuhudia. Tamhilia ni utanzu mmojawapo wa fasihi andishi.

Kwa upande mwingine drama ni utanzu wa sanaa za maonesho inayowasilishwa kwa njia ya uigizaji mbele ya hadhira ambayo pia ni tawi la sanaa tendi. Drama pia inaweza kuelezewa kama wigo wa maisha halisi ya watu katika jamii, licha ya kwamba ndani yake mna ubunifu. Ufafanuzi huu unalandana na ule wa Mumbo (2018) unaorejelea drama kama tawi la sanaa tendi inayowasilishwa kwa njia ya uigizaji mbele ya watazamaji. Drama inaweza kuhusisha tamthilia, ushairi na masimulizi ya hadithi. Kwa hivyo, tofauti ya tamthilia na drama ni kwamba tamthilia huwasilishwa kwa mfumo wa maandishi ya kimajibizano na kuegemea zaidi upande wa fasihi andishi, ilhali drama si lazima iandikwe; inaweza kuigizwa kutokana na utunzi usiokuwa na mswada, matukio ya kimila, utunzi wa kishairi, utunzi wa kimasimulizi na hata utunzi wa tamthilia. Hii ni sanaa iliyo hai. Tamthilia hupata uhai pale tu inapoigizwa mbele ya hadhira. Hata hivyo, tunakiri ya kwamba dhana hizi mbili zinaingiliana pakubwa.

Kwa kuzingatia maelezo hayo, makala haya yametathmini matumizi ya kimya sambamba na sauti kwa kuangazia utendaji kimya na utendaji sauti katika muktadha wa uhusika wa sauti kwenye tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* ya Said A. Mohamed. Hatimaye, asili na chanzo cha matumizi ya sauti katika tamthilia kimewekwa wazi kwa kuzingatia chimbuko la drama katika Uyunani ya kale tangu enzi ya matumizi ya korasi wakati wa maigizo ya kidrama na sanaa za maonesho.

## 2.0 Muhtasari wa Tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya*

Tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* inazungumzia nchi ambayo imekwama kimaendeleo kwa sababu ya uongozi mbaya uliosababisha njaa na madhara ya kila aina, ukiwamo uharibifu wa mazingira kwa miaka mingi. Katika uongozi wa nchi hiyo, wananchi wamedhibitiwa; hawaruhusiwi kusema, wananyanyaswa na kunyimwa haki zao. Tamthilia hii inaanza kwa kuwaonesha wahusika wawili, Kulia na Kushoto, wakiwa wamepotea njia na wamekutana kwenye kisima kikavu chenye maji yasiyotekeka. Kulia anatokea kulia kwa msitu na anaelekea kushoto na Kushoto anatokea kushoto kwa msitu akielekea kulia na wote wawili wana kiu ya karne, lakini hawawezi kupata maji pale kisimani. Mbali na kwamba kile kisima kimekauka, kinatoa sauti na kuwasemesha, jambo ambalo linawatia hofu. Isitoshe, wamekwama pale kisimani, hawawezi kuendelea na safari zao wala kurudi kule wanakotoka.

Baadaye Mpya, binti wa pekee wa kiongozi wa nchi, Bw. Binafsi, anafika pale kisimani na inasemekana kufika kwake pale kulitarajiwa na wahenga. Mpya anajitumbukiza kwenye kisima na kuibuka akiwa amelowa chapachapa huku ameshika bakuli la kunywea maji. Ananyanyua bakuli hilo na kunywa yale maji ambayo anasema ni maji ya ujasiri yanayomtoa hofu na woga. Tukio hili la Mpya kujitumbukiza ndani ya kisima kama alivyoamrishwa na wahenga na kunywa maji ya ujasiri, ni la tambiko la utakaso wa kumwezesha kusema ukweli bila kuogopa. Lilikuwa tambiko la uhai wa nchi za Afrika, tambiko ambalo lilimpa Mpya ushujaa wa kukabiliana na babake bila hofu. Kutokana na ujasiri alioupata kisimani, Mpya aliweza kupambana na babake na kuwaongoza raia kuikomboa nchi yao kutoka katika utawala dhalimu wa babake.

Baada ya Mpya kupokea baraka za wahenga alipata sauti na ujasiri wa kumkosoa babake bila woga na kuwashawishi kaka zake wakubwa, Mussa na Zanga, kuungana naye katika harakati za kudai haki zao na kutaka uhuru wao wa kuongea kama wananchi walioko ndani ya nchi huru. Umma unahamasishwa kuhusiana na umuhimu wa kusema na kudai haki zao, hatimaye, mapinduzi yanatekelezwa yakiongozwa na Mpya, mapinduzi yanayomlazimisha Bw. Binafsi kuondoka mamlakani.

Tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* ni miongoni mwa kazi chache za kisanaa katika lugha ya Kiswahili ambazo zimetumia utendaji sauti kikamilifu katika kiwango cha uhusika, usanii na maudhui. Sauti imepewa uhusika mkuu katika tamthilia hii ambapo inatenda kama wanavyotenda wahusika wengine. Wahusika sauti wanashirikiana kuwasilisha ujumbe kuhusu mageuzi ya kijamii na kisiasa. Wanasisitizia suala la uzalendo na kuleta mapinduzi ya uongozi dhalimu. Mwandishi ameangazia hasa masuala ya kuzingatia uzalendo na kuukemea uongozi mbaya. Kupitia kwa kijana wa kike, Mpya, akishirikiana na ndugu zake, analeta mapinduzi ya uongozi kutoka nyumba au ukoo tawala hadi taifa zima. Katika tamthilia hii mwandishi anaonesha ya kwamba mdongo anamfundisha mkubwa kusema, “Vijana wanawafundisha wazee kusema!” (uk. 54).

## 3.0 Usuli wa Matumizi ya Sauti katika Tamthilia

Matumizi ya sauti katika tamthilia yanahusiana na matumizi ya korasi katika drama za Uyunani ya kale. Mutembei (1995) anafafanua kuwa chanzo cha matumizi ya sauti katika tamthilia kinahusishwa na matumizi ya korasi katika sanaa za maonesho za Wayunani. Korasi katika drama za kirasimi za Uyunani ya kale inaashiria kikundi cha watu ambao walikariri kwa pamoja ili kuelezea matukio yanayofanyika jukwaani wakati wa uwasilishaji wa tamthilia. Mawasilisho hayo yalifanyika kwa njia ya nyimbo, masimulizi na uchezaji ngoma. Banks (1985) akimrejelea Aristotle anasema kwamba tanzia ya Kiyunani ilitokana na korasi, yaani kikundi hiki kilichoigiza kwa pamoja kama kwaya. Kikundi cha korasi kilikuwa na watendaji takriban 50 hivi ambao waliimba na kucheza pamoja wakati

wa matambiko ya matamasha ya kumtukuza mungu wao wa mvinyo na uzazi, Dionysus. Korasi katika sanaa za maonesho za Wayunani ilitekeleza majukumu matatu muhimu; kubainisha muktadha wa utendaji, kutoa muhtasari wa taarifa inyohusu igizo na kutathmini igizo linaloendelea jukwaani kwa hadhira.

Kulingana na Brockett na Hildy (2014), kufikia karne ya 6 Kabla Masihi, inaaminika ya kwamba msanii Thespis alijitoa kutoka katika kikundi cha korasi na akawa mwigizaji wa kwanza kujitenga na kujibizana na korasi katika maigizo. Jukumu la korasi likabadilika, likawa si sehemu ya simulizi ya tanzia tena bali likachukua nafasi ya mhusika wa kidrama; korasi ikawa inajibizana na mwigizaji. Kupatikana kwa mwigizaji kulifanikisha utendaji kwani kuliwezesha kukuza mgogoro wa tanzia. Baadaye, Aeschylus aliongeza mwigizaji wa pili na kila mhusika, kati ya hawa wawili, akawa akichukua nafasi zaidi ya moja. Halikadhalika, Thespis akapunguza jukumu la korasi kwa kupunguza washiriki kutoka 50 hadi 12. Hatimaye, akaanzisha matumizi ya lugha ya majibizano katika tanzia. Sophocles kwa upande wake aliongeza wahusika hadi watatu na matumizi ya mandhari. Sophocles aliipatia korasi umuhimu zaidi kwa kusisitiza kuwa iwepo katika drama lakini isiruhusiwe kudhibiti utendaji.

Kutokana na maelezo hayo, ni bayana kuwa jukumu la korasi katika drama za Wayunani lilipitia mabadiliko polepole ndani ya kipindi kirefu cha kihistoria, kuanzia Uyunani ya kale mpaka leo. Awali, korasi ndiyo iliyokuwa kiini cha tanzia, washiriki walipokuwa wakikariri kwa pamoja katika kikundi, kisha wakawa wanajibizana na wahusika wengine, na mwishoni wakaachiwa nafasi kuelezea kile kinachoendelea jukwaani na kutoa maoni. Hata hivyo, msisitizo wa Sophocles wa kuibakisha korasi katika tanzia ndio uliwafanya wasanii wengine kuipata na kuendeleza matumizi yake na hata kuikuza. Waandishi maarufu wa tamthilia walioendeleza matumizi ya korasi kama sauti ni pamoja na William Shakespeare, Wole Soyinka, Ngugi wa Thiong'o, Ebrahim Hussein na Penina Mulama, kwa kuwataja wachache. Shakespeare alifuata mfumo wa uandishi wa tanzia kama zile za Sophocles ilhali watunzi wa Kiafrika walichukua mifumo na mitazamo mbalimbali.

Katika tamthilia ya Kiswahili suala la matumizi ya sauti katika uwasilishaji wa ujumbe limebainika katika baadhi ya kazi, kama vile *Mashetani* ya Hussein, E. N (1971), *Pungwa* ya Mohamed, S. A (1988), *Kivuli Kinaishi* ya Mohamed, S. A (1990), *Ningekuwa na Uwezo* ya Mkangi, K (2009) na *Mashetani Wamerudi* ya Mohamed, S. A (2016), miongoni mwa nyingine. Katika tamthilia ya *Mashetani* matumizi ya sauti yanadhihirika kupitia kicheko cha kishetani ambacho kinamkejeli Binadamu kwa kupuuza utamaduni wake na badala yake kukubali kila kitu kutoka Ulaya Magharibi. Sauti hii ya kicheko inalenga kumtanababhisha mwanadamu dhidi ya ukoloni mamboleo. Ilhali kwenye tamthilia ya *Pungwa* mwandishi anatumia sauti ya Mzuka kama mhusika anayechukua nafasi ya shetani au pepo ambaye

huwaingia watu akilini na kuwatawala. Huyu ni kiumbe ambaye huwa haonekani kwa macho bali watu huhisi kuwapo kwake, na anapompanda mtu kichwani husababisha kupagawa na kumfanya kuonekana kama mwendawazimu. Pepo hawa ili watolewe, inaaminika lazima wapungwe kwa ngoma, matambiko ama kwa kutoa kafara. Katika tamthilia hii, sauti ya Mzuka ni sauti ya kishetani; ni sauti ya kutisha na inatoka bila kujulikana inakotokea. Katika tamthilia ya *Ningekuwa na Uwezo* utendaji sauti umetumika kumzindua Mwafrika ili aweze kutambua asili na fasili yake. Katika tamthilia hii mwandishi anatumia sauti kuwahimiza Waafrika kujikomboa kimawazo na kujionea fahari vile walivyo pamoja na urithi wao hasa wa kiutamaduni.

### 4.2 Utendaji Sauti

Utendaji sauti umerejelewa kama hali ya kuipa sauti nafasi na uwezo wa kutenda kama wahusika wengine bila ya kuonekana jukwaani. Utendaji sauti unaweza kufanyika kwenye uigizaji wa jukwaani kwa minajili ya kuwasilisha ujumbe kwa hadhira lengwa kama wafanyavyo watendaji wa kawaida katika tamthilia. Kwa hiyo, utendaji sauti ni sanaa ya kuwasilisha mawazo kwa kutumia sauti bila mhusika mwenyewe kuonekana, na pale anapoonekana huoneshwa akiwa katika mawazo au ndoto. Mhusika anayetenda sauti ameelezewa kama mtendaji sauti. Utendaji sauti unatumika sana katika michezo ya redio, drama za runinga, drama za video, filamu, makala, sanaa za vibonzo, kwenye tahariri za redio na runinga na michezo ya jukwaa. Mbali na utendaji sauti katika tamthilia, matumizi ya sauti vilevile yamejitokeza katika baadhi ya kazi za kinathari katika fasihi ya Kiswahili. Baadhi ya riwaya za Kiswahili hususan zile za kifantasia pamoja na hadithi fupi zimetumia utendaji sauti kuibua hisia, mawazo na mitazamo mbalimbali katika jamii. Hata hivyo, ni katika tamthilia na drama ambapo utendaji sauti unatumika kwa namna maalum na ya kipekee.

Alburger (2011) anaeleza kwamba utendaji sauti huwa na jukumu muhimu la kuburudisha, kutangaza na kuuza bidhaa pamoja na kuwasilisha habari. Utendaji sauti huwa na jukumu la kutenda kile ambacho kimeandikwa kwenye mchezo wa kuigiza. Ili kufanikiwa katika kufanya hivyo, mtendaji sauti sharti afahamu namna ya kuwasilisha sauti hiyo bila kusitasita ili ujumbe utolewe ipasavyo kwa kutumia sauti pekee, kwani huwa hatumii viziada lugha kama mwigizaji aliyezoeleka. Jukumu la utendaji sauti ni kuwasilisha ujumbe na kuufanya kuwa na uhalisia iwezekanavyo ili kuathiri hadhira kihisia na kumfanya msikilizaji kuukumbuka ujumbe husika.

Mara nyingi utendaji sauti unapotumika katika tamthilia unakiuka ile mipaka ya kiuhalisia. Katika hali hiyo mhusika huwa anapewa sauti ambayo si ya kawaida kwa sababu mtunzi huwa analenga kuibua hali na hisia maalumu. Kwa mfano, wakati mwingine mhusika anaweza kutoa sauti ya Mungu, sauti ya mizimu, sauti ya kishetani, sauti ya mtoto ambaye yuko tumboni mwa mamake na kadhalika. Hata

pale sauti za kawaida zinapotumika, wakati mwingine zinatiwa chumvi ili kufikisha hisia maalumu. Wahusika sauti wanaojitokeza katika tamthilia ya *Kimya kimya Kimya* ni pamoja Sauti Ndani ya Kisima, Sauti ya Mpya na Sauti ya Umma ambao tumewajadili katika sehemu ya 5.0.

### 4.3 Mtendaji Sauti

Mtendaji sauti ni mhusika anayeigiza au kuwakilisha sauti iliyotumiwa katika mchezo wa kuigiza au tamthilia. Dhima yake kuu ni kuchukua uhusika wa sauti kama ilivyotumika katika tamthilia mahususi na kuiwasilisha. Huyu ni mhusika ambaye anaipa uhai sauti hiyo kupitia kutenda, na katika utendaji huo, anadhihirisha hali, msimamo, mwelekeo pamoja na kufikisha ujumbe uliokusudiwa kuwasilishwa na sauti husika. Ili mtendaji sauti afanikiwe kutenda sauti husika anapaswa kuelewa hadhira yake, wahusika wengine waliolengwa katika sauti hiyo pamoja na dhima ya sauti inayoigizwa. La muhimu zaidi ni kwamba mtendaji sauti inambidi kuelewa namna ya kuiigiza sauti hiyo. Kwa hiyo, mtendaji sauti katika tamthilia ni yule mhusika anayeoneshwa kwa maandishi kama sauti na katika drama ni yule mwigizaji aliyepewa jukumu hili ili kulitekeleza jukwaani.

Fisher na Hogan (2005) katika mwongozo wa mtendaji sauti, wanashughulikia namna ya kurekodi sauti kama mtendaji. Wanaangazia jinsi watendaji sauti chipukizi na wale weledi wanavyoweza kutumia makazi yao kurekodi utendaji sauti kwa ajili ya miradi mbalimbali ya uigizaji kwenye mashirika makubwa ya drama, vituo vya redio, michezo na vipindi vya runinga hasa katika mataifa yaliyoendelea. Hata hivyo, mjadala wetu umejikita katika kuangazia namna sauti ilivyotumika kama mhusika na namna sauti mbalimbali zinazobainika katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* na zinavyotumiwa kufanikisha maudhui yaliyomo.

Hivyo basi, mtendaji sauti ni mhusika anayejengwa kwa misingi ya kiuhalisia ili aweze kuaminika katika hali, mazingira na muktadha kwa mujibu wa dunia aliyowaumbia mtunzi. Ujumbe unaowasilishwa na mtendaji sauti hutawaliwa na hisia na huwa na lengo maalumu; kwa hivyo, ni sharti aweze kuathiri hadhira kihisia katika mawasiliano yake.

## 5.0 Uhusika wa Sauti katika Tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya*

Sauti ambazo tumezibainisha na kuzijadili katika kazi hii ni pamoja na sauti yenyewe, Sauti ya Mpya, Sauti ya Kimya, Sauti ya Kisima na Sauti ya Umma.

### 5.1 Sauti ya Kisima

Mwandishi ameitumia sauti ya kisima katika kujenga uhusika na maudhui. Kupitia utendaji wa sauti kisimani, mwandishi anaelezea umuhimu wa kisima kwa jamii. Kisima hiki ni cha zamani, tangu jadi watu walikimbilia hapa walipokumbwa na matatizo mbalimbali katika jamii ili wapate suluhisho. Anasema kwamba kisima hiki ni kitakatifu, ambapo wahenga walikutana kujadili mateso na kutafuta njia ya

kuyaondoa. Hapa ndipo pahala palipochotwa maji ya kukata kiu na kuzima joto lililokuwamo ndani ya nafsi za watu. Ndipo wazee walipoenda kupata mori wa kusonga mbele na kuzisemesha nafsi zao zilizodidimizwa na wageni kwa muda mrefu. Ndipo hapohapo Fumo Liyongo alipofia. Ijapokuwa kisima ni ishara ya uhai, chemchemi ya maisha, msukumo wa maendeleo ya jamii na ishara ya mwelekeo wa jamii na kiini cha jamii, vilevile kinaweza kuwa maangamizi ya jamii.

Hivyo basi, sauti inayotoka kisimani inabainisha utendaji wa kidrama na kutokana na uhusika huo, ujumbe muhimu unawasilishwa kwa hadhira. Sauti Ndani ya Kisima inatumiwa kama mhusika anayetagusana na wahusika wengine ili kuwasilisha maudhui ya uzalendo, mageuzi, ukombozi, kupigania haki za wananchi wote bila ubaguzi, kuishi kwa umoja na utangamano kwa kujali maslahi ya kila mtu katika nchi nzima. Haya ni baadhi ya maudhui yanayowasilishwa kupitia sauti ya kisimani katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya*. Sauti katika hali hii inachukua nafasi muhimu katika kuwasilisha mawazo kwa walengwa. Tazama dondoo lifuatalo la Sauti Ndani ya Kisima:

> Hakuna uhai. Hakuna chakula. Hakuna maji. Hakuna ari ya kusema. Hakuna shime ya kutenda. Hakuna mori wa kukataa. Hakuna ushinde wa kushindana na kuchachamaa ili kujikwamua... Tazama mbele, usitazame nyuma. Ijali tamu ya nchi, usijali tamu ya siasa tupu. Ijali nchi na kuitetea (uk. 8).

Sauti hii inasisitiza uzalendo, kuijali nchi na wananchi wake kuliko siasa tasa, siasa mbaya ya kubomoa nchi inayozaa hali ya mateso na kuwatamausha watu wake maishani. Kauli hii inasisitizwa kwa kurudiwa tena na kisima hiki kinaposema:

> Ulikopita kote kukavu. Kote kumedamirika. Hakuoti kitu. Hakuzai kitu. Huko nafsi za watu zimefifia ari. Hata ya kusema neno moja la kweli, neno moja la utetezi... Tazama mbele, usitazame nyuma. Ijali tamu ya nchi yako usijali tamu ya siasa (uk. 11).

Kisima kinatuasa tusahau yaliyopita na tugange yajayo; tuwe wazalendo wanaojali nchi yao. Aidha, tujiepushe na siasa mbaya inayoleta maangamizi.

Mpya, mhusika mkuu, anasawiriwa kama mwanamke mzalendo ambaye amezinduka na mwenye ari ya kuipigania nchi yake, licha ya kwamba kiongozi mbaya anayewadhulumu wananchi ni baba yake mzazi. Mpya ni msichana ambaye umri wake ni mdogo lakini hilo halimzuii kwenda kinyume na babake katika kupigania haki ya wananchi, yaani umma. Sauti inayomzungumzia kutoka kisimani inampa ujasiri na msukumo wa kuikomboa nchi yake kama inavyoonekana hapa chini:

> Ishara njema...Ishara njema...Ishara njema...Njema, njema, njema, ishara njema. Tulikutaraji. Sasa wakati umeshafika. Njoo uliyekuwa ukitarajiwa. Njoo uliyengijewa. Njoo, njoo, njoo...njoo polepole, njoo

> kwa uhakika, njoo tukunyweshe maji ya ujasiri. Ingia ndani ya kisima, uogelee na kujisuuza (uk. 21).

Sauti kutoka ndani ya kisima inamhimiza Mpya kupigania haki za watu wanaonyanyaswa katika jamii yake ili kubadilisha mkondo wa maisha yao. Kisima kinamwambia kwamba yeye ndiye amekuwa akisubiriwa ili kuibadili hali ya jamii yake. Ajitumbukize kwenye kisima apate ujasiri wa kuyatekeleza hayo. Baada ya kujitumbukiza katika kisima hiki, ndipo Mpya anapopata ujasiri wa kuleta mageuzi yanayohitajika katika jamii yake. Kisima hiki kimepewa jukumu, kupitia sauti yake, kuangazia maudhui ya uzalendo na kujitoa mhanga kwa manufaa ya nchi nzima. Katika kisima, Mpya alipitia mabadiliko kwa kutakaswa na kutolewa uovu wote unaotokana na aila yake na kisha kupewa ujasiri uliomfanya kuibuka kama mtu shupavu na shujaa.

### 5.2 Sauti ya Mpya

Yapo matukio katika tamthilia hii ambapo mhusika Mpya hatendi wala kusema kama anavyosawiriwa na mwandishi. Sauti yake inapewa nafasi ya kuisemesha hadhira kwa niaba yake. Huyu ni Mpya ambaye ameshasafishwa na kupata ujasiri baada ya kujitumbukiza kwenye kisima. Alioshwa, akaosheka na kuzinduka kiasi kwamba sasa alikuwa tayari kusema na kulikabili jukumu lake jipya la kuongoza mageuzi. Kwa hivyo, alikuwa mpya kwa maana halisi ya upya. Sauti hiyo ya Mpya inajidhihirisha kama ifuatavyo:

> Huyu ndiye baba’ngu. Mtu wa ajabu! Nafsi yake ni yake mwenyewe. Lakini nafsi zetu si zetu...nafsi zetu ni...aaa sisemi...siruhusiwi kusema! Nimechoka kusubiri. Nimechoka kungojea. Nimechoka kunyamaza! Huku kunyamaza najua ndiko kunakoniangamiza mimi na wote nchini humu. Ulimi unaniwasha (kur. 30 - 31).

Katika dondoo hilo, Mpya anaonekana ameketi kwenye meza ya maakuli, yeye na familia yake. Hazungumzi na yeyote, bali sauti hii inatoka nyuma ya jukwaa na inasikika na walio mezani. Sauti yake hii inadhihirisha uongozi wa kiimla wa babake. Nafsi ya kila mtu ni yake lakini yake ni yake mwenyewe. Hakuna anayeruhusiwa kusema kinyume na matakwa ya Bw. Binafsi. Sauti hii inatudhihirishia kwamba Mpya amezinduka. Yuko tayari kukiuka kanuni hizo za babake. Hapa ndipo uhasama kati yake na babake unapoanza. Hili ni zao la utendaji wa Sauti ya Mpya, yeye mwenyewe hasemi lakini sauti yake inasikika kote.

Bw. Binafsi anajisifu namna familia yake hii inavyomtegemea kwa kila hali na kumkaripia Mpya kwa kutaka kuutia dosari ubaba wake. Sauti ya Mpya inajibu kwamba ni matendo yake, Bw. Binafsi ndiyo mbaya. Sauti hiyo inasikiwa na Bw. Binafsi pekee ambaye naye anaijibu sauti hiyo kama ifuatavyo:

> Sitaki kuingiliwa kati mimi nikisema... Mimi namsikia ndani ya kichwa chake. Namsikia kupitia uso wake. Kupitia macho yake. Kupitia nia yake... (*Kicheko cha Mpya*.) Ha, ha, ha, ha...(*Kicheko cha muda wa haja*

> *kinakuja mfululizo kutoka nyuma ya jukwaa. Lakini Mpya anaonekana kasawijika. Ana huzuni nyingi. Kamwe hacheki! Wala hasemi. Mpya haonekani kucheka kamwe.*)
> Mnaona ananicheka? (Uk. 40).

Katika mfano huo, mapinduzi yanadhihirika. Mpya, kwa mara ya kwanza kama sauti yake inavyodhihirisha, amemsemesha baba yake. Hamwogopi tena. Mapinduzi yameanza kwenye kina chake, nyumbani kwa kiongozi mwenyewe. Huu ndio mwanzo wa harakati za Mpya za kuleta mapinduzi, ndani na nje ya nyumbani kwao. Aidha, katika kur. 50 - 51 sauti ya Mpya inasikika:

> Kila siku vitu vingi huanza kama mchezo. Kama wasemavyo wazee: mwanzo wa ngoma ni lele. Lakini jambo hili la kusema na kutetea haki zetu si langu peke yangu. Mimi mnayeniita mtoto! Hili ni jambo letu sote, watu wazima, vijana na hata watoto. Ni jambo nyeti lisilotaka kufanyiwa mzaha. ninafarajika kwa hivyo kuona kwamba mnalichangamkia na kuliunga mkono.

Katika mfano huu sauti ya Mpya inasema na kaka zake, ambao ndio wameanza kushabikia suala la kuleta mabadiliko. Wamepata ujasiri wa kutetea haki zao, uwezo ambao walikuwa wamenyimwa na baba yao mzazi kwa muda mrefu kama Sauti ya Mpya inavyodhihirika hapa chini.

> Kweli kuliko kweli yoyote. Kweli kama lilivyo jina langu. Zaidi ni kwamba wamenituma nije kukufahamisheni ukweli ili muwe pamoja na umma. Wazee na vijana lazima washikane kutetea haki yetu ya kusema. Tuseme ukweli hadi udhihiri na uwongo upate kujitenga... (uk. 54).

Mpya anawaambia kaka zake Zanga na Mussa kuwa ametumwa na wazee awahimize washirikiane na umma ili vijana na wazee washikane pamoja kupigania haki zao za kusema. Wapambane kusema ukweli mpaka wauondoe uwongo. Kwa hiyo, Mpya anawahamasisha ndugu zake kujiunga na wananchi wengine katika kutetea haki zao. Hatimaye wanazinduka na kuongoza mapinduzi yanayotokea.

Hivyo, mwandishi ametumia sauti ya Mpya kupendekeza mabadiliko ambayo wananchi hawa wanayahitaji. Kwanza kabisa, anapendekeza mageuzi ya katiba kwa mujibu wa matakwa ya nchi na ya kimataifa. Pili, watu wabadili mienendo yao ya kutojali na kutothamini maslahi yao ya kitaifa na badala yake kukumbatia zaidi maslahi mataifa ya nje. Tatu ni mabadiliko yatakayohakikisha kuwa wananchi wanapata huduma za kijamii katika nchi yao. Nne, kupigana vita dhidi ya ufisadi na kuhakikisha ya kwamba wawekezaji na makampuni makubwamakubwa kutoka nchi za nje yanalipa kodi kama inavyostahili. Tano, tuweze kulinda rasilimali kutokana na wizi wa kiholela. Maudhui yote haya yanawasilishwa kwetu na uhusika wa sauti ya Mpya.

**5.3 Sauti ya Umma**

Mwamko mpya umetoka ndani ya nyumba ya kiongozi mwenyewe na kuzagaa nje. Wananchi, kwa umoja wao, wameungana katika kuleta mabadiliko wanayoyataka kama tulivyoeleza hapo juu. Raia wanalalamika kwamba matakwa yao hayatiliwi maanani na viongozi kwa muda wa miaka hamsini tangu kupata uhuru; kwa hiyo, wamejitolea kufanya maandamo kwa njia ya amani ili kuushinikiza uongozi kutekeleza mahitaji yao kama Sauti ya Umma inavyojibainisha:

> Tumekubali. Tumekubali yote. Tuko pamoja na wewe. Tuko tayari. Tuko tayari kuingia njiani kwa nidhamu nzima. Bila ya uchokozi, bila fujo. Iwapo matakwa yetu hayasikilizwi licha ya kutekelezwa kwa miaka hamsini, sisi wananchi hatuna budi kuingia barabarani kusema kwa amani... (uk. 73).

Wananchi wanakubali kuungana na kushirikiana pamoja na Mpya katika juhudi za kutetea haki zao. Katika hatua hii, mawazo ya wananchi na yale ya Mpya yanaoana. Kwa hivyo, wote wanaridhia kufanya maandamano ya amani hadi pale watakaposikilizwa na haki zao kutimizwa. Wananchi hapa wanadhihirisha umoja wao katika kudai haki zao na hata zaidi wanaposema kwamba:

> Sauti yako inatueleza tunayoyajua. Sauti yako ni sauti yetu kwani wewe ni sisi na sisi ni wewe. Wewe na kaka zako mmefukuzwa nyumbani, lakini nyinyi mna nyumba zote za nchi hii-mnakaribishwa, karibuni. Usiwe na wasiwasi, tutaingia barabarani kimya kimya bila fujo. Tutaingia kimya kimya. Tutaingia kwa amani. Hatusiti mpaka sauti zetu zisikike (uk. 75).

Sauti hii imepewa jukumu la kuwasilisha maudhui ya umuhimu wa umoja wa kitaifa na njia za amani za kutetea haki. Wananchi kupitia sauti yao, wanatekeleza haya, na katika kufanya hivyo wanasafisha taifa na kulitakasa. Hatimaye, kupitia juhudi hizo na kutokata tamaa, wananchi wanafanikiwa kuleta mapinduzi ya amani, mapinduzi ya kimya.

**5.4 Sauti Yenyewe**

Mbali na utendaji sauti unaowakilisha baadhi ya wahusika na matukio mbalimbali katika kazi hii ya sanaa, mwandishi ametumia sauti nyingine ili kuwasilisha mawazo aliyokusudia kwa hadhira. Miongoni mwa sauti hizo ni zile ambazo tumezieleza kama sauti zenyewe. Kwa mfano, kuna sauti ya mkemeo inayotokana na mhusika fulani kuwatolea watu wengine maneno kwa ukali, kukaripia ama mhusika mmoja kuamrisha (m)wengine. Zingatia sauti zifuatazo:

> Mkemeo: Kimyaaaaa! Kimyaaaaa! Kimyaaaaa! Nyamazeni!
> (Kimya! Halafu kitambo! Bado giza vilevile! Bado kimya.
> Mkemeo na mkaripio zaidi unaamrisha hadhira!)
> Nasuma kimya! Hamsikii? (uk. 26).

Sauti: A-a, Bi. Mpya, hapa kwenu watu hawasemi waziwazi wala hawasemi kwa kelele. Hawaruhusiwi kufanya hivyo! (uk. 27).

Mpya: Mimi nimeanza.
Sauti: Wewe nani?
Mpya: Mimi mwananchi. Mimi mzalendo. Mimi mkereketwa.
Sauti: Hapana, wewe ni raia wa familia hii inayoongoza nchi. Wewe ni mtoto wa Mzee Binafsi, babako na Bi Shoo, mamako (uk. 28).

Mkemeo huu unasikika mwanzoni mwa onesho la pili la tamthilia hii ya *Kimya Kimya Kimya*. Hapa ni nyumbani kwa Bw. Binafsi ambapo watu hawana uhuru wa kusema; wanasema tu wanapopewa fursa na wanasema tu kile ambacho kinanuiwa kumfurahisha kiongozi wa nyumba hiyo. Hali hii inadhihirisha uongozi dhalimu, wa kiimla na wenye kuwakandamiza watawaliwa kama vile, wananchi kunyimwa haki ya kusema hata pakiwa na haja ya wao kufanya hivyo. Kukithiri kwa jambo hili la watu kunyimwa uhuru wa kujieleza kunajitokeza pale ambapo hata katika aila yake mwenyewe hakuna anayeruhusiwa kusaili chochote. Majibizano kati ya Bw. Binafsi na binti yake Mpya yanatudhihirishia hilo.

Pamoja na sauti, mwandishi vilevile ametumia milio kiishara ili kuwasilisha ujumbe kuhusu mapinduzi yaliyokuwa yanauandama uongozi wa Bw. Binafsi. Kupitia mlio mkali ambao ulitokana na mporomoko wa vitu vingi jikoni vikiwamo vile vya chuma, mwandishi alinuia kuwasilisha ujumbe maalum. Mlio mkali wa mpasuko na kuanguka kwa vyombo jikoni uliosababishwa na upepo mkali uliokuwa ukivuma uliangusha vitu vizito vya chuma na kumfanya Bw. Binafsi kuelekea mbio jikoni ili apate kujua kitu kilichokuwa kikiangusha na kuvunja vyombo hivyo. Alipotanabahi akaambiwa ulikuwa upepo unapiga kwa nguvu. Tukio hili linabashiri kuanguka kwa utawala wa kiimla wa Bw. Binafsi na mwanzo mpya, mwanzo wa mabadiliko ya kweli katika utawala wa kisiasa, hali ya kijamii na ya kiuchumi. Upepo unaovuma ni harakati za wanawe zikiongozwa na Mpya, Zanga na Mussa, ambao tayari wameungana na umma katika kutetea haki zao.

**5.5 Sauti ya Kimya**

Hii ni kinaya kwamba kimya kinasema kwa kuwa katika hali halisi, kimya hakiwezi kusema wala kutoa sauti, na ndio maana ni kimya. Hata hivyo, katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya*, kimya kimepewa nafasi ya kushiriki, kuzungumza na kutoa sauti. Kimya kimejengwa kama mhusika na kupitia utendaji wake tunapata maudhui mbalimbali. Sauti zote tulizozijadili zinasikika kupitia kimya. Kwa mfano, Sauti ya Mpya inaposikika, yeye mwenyewe yupo kimya, hasemi. Sauti ya wahenga inaposikika ndani ya kisima, kisima hakisemi. Hivyo, sauti hizi zote zinasikika kimyakimya. Kwa mfano, mwandishi anaeleza kwamba malalamiko ya kimyakimya yanatokea akilini mwa Mpya (uk. 29).

Sauti ya wananchi nayo, kama tulivyoeleza hapo juu, inakiri kwamba wananchi hawatasita mpaka watakaposikika; wataandamana barabarani kimyakimya. Kwa mujibu wa tamthilia hii, utendaji sauti na kimya vimefungamanishwa na kusukwa kiufundi ili kufanikisha utoaji wa ujumbe uliokusudiwa kwa hadhira. Hivyo, ni bayana kwamba hata katika ukimya utendaji unadhihirika. Makundi mbalimbali ya sauti tulizobainisha yanasema na kusikika kimyakimya. Hata sauti yenyewe inasema kimya kimya kimya.

**6.0 Hitimisho**

Hatimaye utendaji sauti unaweza kuelezwa kama njia ya usanii ya kuwasilisha ujumbe kwa kutumia sauti bila wahusika wenyewe kudhihirika jukwaani, yaani kuipa sauti uhusika na uwezo wa kutenda matukio fulani mbele ya hadhira. Sauti katika tamthilia ya *Kimya Kimya Kimya* imepewa uhusika mkuu wa kuwasilisha ujumbe muhimu kwa jamii. Hivyo basi, sauti imetekeleza jukumu muhimu sana katika kufanikisha tathmini ya wazo kuu linalowasilishwa katika tamthilia hii. Maudhui mbalimbali yamebainika yakiwamo yale ya mageuzi ya kisiasa, mageuzi ya kijamii, uzalendo na utaifa, mapambano dhidi ya ufisadi pamoja na kupigania haki za wananchi. Mapinduzi yaliongozwa na vijana na yalianzia katika nyumba au nasaba tawala. Katika makala haya tumeonesha namna ambavyo sauti imeweza kutekeleza jukumu la uhusika na kutenda au kuigiza nafasi mbalimbali katika tamthilia. Utendaji huu wa sauti ni wa kipekee katika utendaji wa kidrama na uwasilishaji wa matukio katika jukwaa, hasa kwa kuwa sauti hizi zinasema Kimya! Kimya! Kimya! katika kuwasilisha ujumbe. Fani ya kinaya iliyolenga kubainisha namna ambavyo kimya kinaweza kusema na kutoa sauti zenye kusababisha mageuzi, imetumika kwa njia mwafaka.

**Marejeleo**

Alburger, J. (2011) *Voice Acting: The Craft and Business of Performing for Voice-Over*. Masachussets: Focal Press.

Banks, R. A. (1985) *Drama and Theatre Arts*. London: Hodder and Stoughton Ltd.

Brockett, O. G. na Hildy, F.J. (2014) *History of the Theatre*. Tenth Edition. London: Pearson Educational Books.

Fisher, P. J. na Hogan, H. (2005) *The Voice Actor's Guide to Home Recording*. Masachussets: Boston.

Goldfarb, A and Wilson, E. (2002) *Theatre: the Lively Art*. New York: McGraw Hill Companies.

Habwe J. na Zaja J. O. (2019) *Kamusi ya Isimu na Fasihi*. Nairobi: JKF

Hogan, H. (2002) *VO: Tales and Techniques of a Voice-Over Actor*. New York: Allworth Press.

Hussein, E. N. (1971). *Mashetani*. Nairobi: Oxford University Press.

Hutton, J. (1982) *Aristotle's Poetics*. New York. London: W.W. Norton & Company.

Khamis, S. A. M. (2007) "The Swahili Novelist at The Crossroads: The Dilemma of Identity and Fecundity". *Swahili Forum* Juz. Na.14: 165-180.

Mkangi, K. (2009) *Ningekuwa na Uwezo*. Nairobi: Oxford University Press.

Mohamed, S. A. (2016) *Mashetani Wamerudi*. Nairobi: Spotlight Publishers (EA) Ltd.

Mohamed, S. A. (2011) *Kimya Kimya Kimya*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Mohamed, S. A. (2001) *Babu Alipofufuka*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Mohamed, S. A. (1990) *Kivuli Kinaishi*. Nairobi: Oxford University Press.

Mohamed, S. A. (1988) *Pungwa*. Nairobi: Longman Kenya Ltd.

Msigala, S. H. (2021) "Korasi katika Filamu za Kiswahili". *Mulika,* Juz. Na. 40 (1): 126-146.

Mumbo, C. K. (2019) "Uchunguzi wa Kidrama wa Riwaya ya Kiswahili na Maendeleo ya Fasihi Afrika Mashariki: Unaitwa Nani? K.W. Wamitila". *Mwanga wa Lugha*: 105-120.

Mumbo, C. K. (2018) "Urazinishaji wa Mwafrika: Tafakuri ya Drama ya Kiswahili". Katika M.

Mukuthuria na M. Kandagor (Wah.) *Fasihi ya Kiswahili: Utafiti na Maendeleo Yake*. Dar es Salaam: TATAKI. kur. 239-255.

Mutembei, A. K. (1995) "Korasi na Uhusiano wake na Sanaa za Maonyesho: Uchunguzi wa Kidayakronia". *Kioo cha Lugha,* Juz. 2:67-73.

Mutembei, A. K. (2012) *Korasi Katika Fasihi: Nadharia Mpya ya Uhakiki*. Dar es Salaam: TUKI.

Wafula, R. M. (1999) *Uhakiki wa Tamthilia. Historia na Maendeleo Yake*. Nairobi: JKF.

Wamitila, K. W. (2003) *Kamusi ya Fasihi Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Books.

Willet, J. (1978) *Brecht on Theatre*. London: Eyre Methuen.